TANGAZO LA SERIKALI NA. 385 la tarehe 2/6/2023

SHERIA YA HAKIMILIKI NA HAKISHIRIKI,
(SURA YA 218)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 48A)*

KANUNI ZA ADA YA HAKIMILIKI KWA VIBEBEO VYA KAZI ZA UBUNIFU VILIVYO TUPU ZA MWAKA 2023

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni Maelezo*

1. Jina la Kanuni.
2. Tafsiri.
3. Ada ya hakimiliki.
4. Malipo ya ada.
5. Ukusanyaji wa ada.
6. Mgawanyo wa ada.
7. Utunzaji wa kumbukumbu na ukaguzi.
8. Utaifishaji na ufungiaji wa majengo.
9. Makosa na adhabu.

*Tangazo La Serikali Na. 385 (Linaendelea)*

SHERIA YA HAKIMILIKI NA HAKISHIRIKI,
(SURA YA 218)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 48A)*

KANUNI ZA ADA YA HAKIMILIKI KWA VIBEBEO VYA KAZI ZA UBUNIFU VILIVYO TUPU ZA MWAKA 2023

Jina la Kanuni

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Ada ya Hakimiliki kwa Vibebeo vya Kazi za Ubunifu Vilivyo Tupu za mwaka 2023.

Tafsiri

**2**. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada ya hakimiliki" au "ada" maana yake ni ada inayotozwa kwenye vibebeo vilivyo tupu kwa mujibu wa kifungu cha 48A cha Sheria;

"kampuni" maana yake ni kampuni za kukusanya na kugawa mirabaha;

"kibebeo kilicho tupu" maana yake ni kitu, chombo au kifaa kisichokuwa na kitu ndani yake, kinachotumika au kinachoweza kutumika kunakili au kuhamisha kazi ya ubunifu inayolindwa;

"Ofisi" maana yake ni Ofisi ya Hakimiliki ya Tanzania iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 46 cha Sheria;

Sura ya 218

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya hakimiliki.

Ada ya hakimiliki

**3**. Kwa kuzingatia kifungu cha 48A cha Sheria, ada ya hakimiliki itatozwa kwenye thamani ya vifaa vilivyo tupu vifuatavyo:

(a) redio au televisheni inayorekodi;

(b) kinasa sauti cha analojia;
(c) kinasa video cha analojia;
(d) kifaa cha kunakili data katika CD au DVD;
(e) kifaa kinachotumia mfumo wa kompyuta wa kuweka mafaili ya muziki;
(f) kifaa cha kusikilizia MP3.

Malipo ya ada

**4**. Ada inayopaswa kulipwa chini ya Kanuni hizi -
(a) kwa vibebeo tupu vilivyotengenezwa, vilivyozalishwa au kuunganishwa nchini, italipwa na mtengenezaji wa vibebeo hivyo; na
(b) kwa vibebeo tupu vilivyoingizwa nchini kutoka nje ya nchi, italipwa na muingizaji wakati wa kuviingiza nchini.

Ukusanyaji wa ada

**5**.-(1) Ada ya hakimiliki itakusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kuzingatia utaratibu wa kawaida wa ukusanyaji wa mapato.

(2) Ada itakayokusanywa chini ya kanuni hii itawekwa katika akaunti ya benki iliyofunguliwa na Ofisi kwa ajili ya ada hiyo.

(3) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa kanuni ndogo ya (2), Ofisi itaitaarifu Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa maandishi kuhusu akaunti ya benki ambamo ada iliyokusanywa itawekwa.

Mgawanyo wa ada

**6**.-(1) Ofisi italipa malipo yanayofaa kwa mtu mwenye hakimiliki au kampuni kutoka katika ada iliyokusanywa chini ya Kanuni hizi kwa kuzingatia mgawanyo ufuatao:
(a) asilimia kumi kwa ajili ya Mfuko wa Utamaduni na Sanaa;
(b) asilimia ishirini kwa ajili ya uendeshaji wa Ofisi;
(c) asilimia kumi kama gawio kwa Serikali; na
(d) asilimia sitini itagawiwa sawa miongoni mwa kampuni zote za kukusanya na kugawa mirabaha.

(2) Kampuni zitagawa malipo kwa ajili ya kazi za muziki, kazi zinazosikika na kuonekana na kazi za fasihi kwa mujibu wa Kanuni za Mgawanyo zilizoidhinishwa na Ofisi.

Utunzaji wa kumbukumbu na ukaguzi

**7**. Mtu anayejihusisha na utengenezaji, uunganishaji au uingizaji nchini wa kifaa chochote kinachopaswa kulipiwa ada ya hakimiliki-

(a) atatunza vitabu na kuwasilisha taarifa kwa vipindi maalum kadri itakavyohitajika na Ofisi;

(b) atamruhusu mkaguzi wa hakimiliki kwa wakati unaofaa kufanya ukaguzi wa eneo lake.

Utaifishaji na ufungiaji wa maeneo

**8**. Endapo ada haijalipwa na mtengenezaji, muunganishaji au muingizaji nchini wa vifaa kama inavyoelekezwa katika Kanuni hizi, Ofisi au Mamlaka ya Mapato Tanzania inaweza kuzuia mzigo wowote wa vifaa vinavyopaswa kulipiwa ada, na pale itakapoonekana ni muhimu, inaweza kufunga eneo lolote linalotumika kwa ajili ya kutengeneza, kuunganisha au kuhifadhi vifaa hivyo kwa kipindi ambacho ada itakuwa haijalipwa.

Makosa na adhabu

**9**. Mtu yeyote anayekiuka Kanuni hizi anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kwa adhabu zilizoainishwa katika Sheria.

Dodoma,
18 Mei, 2023

PINDI H. CHANA
*Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo*